
JARIDA
SEKRETARIETI YA AJIRA

**Toleo namba 2 - August 2024** | *Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma*

# Waziri Simbachawene na Kikwete wazindua mfumo mpya wa usaili kidigitali





*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene akiwa na Kaimu Katibu wa PSRS Bw. Innocent Bomani Wakifatilia namna usaili kidigitali unavyofanywa na moja ya wasailiwa wa Kada ya TEHAMA mkoani Manyara wakiwa wameambatana na Naibu Katibu Miundombinu ya TEHAMA Bi. Mtage Ugulum na Kaimu Mkuu wa Chuo cha VETA Babati Bi Nansanga Massangya.*

## HABARI KUU

1. Waziri Simbachawene na Kikwete wazindua mfumo wa usaili kidigitali
2. Miaka 60 ya Muungano; Simbachawene aipongeza Sekretarieti ya Ajira
3. Watumishi wa Sekretarieti ya Ajira wapewa mafunzo ya PEPMIS
4. Sekretarieti ya Ajira yatoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari nchini
5. Watumishi PSRS wapewa mafunzo ya NeST

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene amezindua mfumo mpya wa usaili kidigitali ujulikanao kama Online Aptitude Test System (OATS) ambao umeanza kutumika kwa mara ya kwanza nchini Tanzania.

Mhe. Simbachawene aliuzindua mfumo huo tarehe 6 Aprili 2024 katika kituo cha usaili kidigitali Chuo cha Ufundi Stadi VETA wilayani Babati Mkoani Manyara, ambapo kwa mara ya kwanza nchini usaili huo wa kidigitali ulifanyika nchini Tanzania

Wakati huohuo Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete

*Inaendelea Uk 2*

## Bomani aelezea mafanikio ya Sekretarieti ya Ajira miaka mitatu ya Rais Samia



*Kaimu Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw. Innocent Bomani*

Kaimu Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Bw. Innocent Bomani amesema kuwa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ametekeleza mambo mengi makubwa katika miaka mitatu ya uongozi wake, ambapo ametoa ajira nyingi sana.

Bw. Bomani amesema kuwa katika miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan ajira zimetolewa kwa makundi mengi ikiwemo makundi ya watu wenye mahitaji maalumu (walemavu) ambapo wamepata ajira kwa wingi na kupangiwa katika taasisi mbalimbali za umma.

## 'Mfumo wa OATS unaenda kuwasaidia Watanzania'- Kikwete'



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Mhe.Ridhiwani Kikwete*

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Ajira na Vijana Mhe. Ridhiwani Kikwete amesema kuwa kuanzishwa kwa mfumo wa Usaili Kidigitali, OATS ni kielelezo cha namna Rais Samia Suluhu Hassan ameendelea kufanikiwa kuwafikia kundi la vijana ambao wamekuwa wakitafuta ajira.

Mhe. Kikwete amesema wapo vijana walikuwa wanashindwa kuzifikia fursa za ajira kwa sababu ya umbali wanapoishi, lakini sasa mfumo huu unaenda kuwasaidi kwenye eneo hilo la ajira

# Waziri Simbachawene na Kikwete wazindua mfumo wa usaili kidigitali

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene amezindua mfumo mpya wa usaili kidigitali ujulikanao kama Online Aptitude Test System (OATS) ambao umeanza kutumika kwa mara ya kwanza nchini Tanzania.

Mhe. Simbachawene aliuzindua mfumo huo tarehe 6 Aprili 2024 katika kituo cha usaili kidigitali Chuo cha Ufundi Stadi VETA wilayani Babati Mkoani Manyara, ambapo kwa mara ya kwanza nchini usaili huo wa kidigitali ulifanyika nchini Tanzania.

Wakati huohuo Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete alizindua mfumo huo akiwa katika moja ya vituo vya usaili kidigitali ambacho ni Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph kilichopo jijini Dar es Salaam.

Mhe. Waziri Simbachawene aliongozana na Kaimu Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw. Innocent Bomani ambao kwa pamoja walipokelewa na Kaimu Mkuu wa Chuo cha Veta Babati Bi Nansanga Massangya ambapo usaili huo wa kidigitali kwa Mkoa wa Manyara ulifanyika katika kituo hicho.

Mfumo huo unawawezesha wasailiwa wote nchini kufanya usaili katika Mikoa wanapoishi bila ulazima wa kusafiri kwenda Mikoa mingine kufanya usaili wa kuandika kama ilivyokuwa hapo awali. Akizungumzia usaili huo, Mhe. George Simbachawene alisema kuwa kwa mara ya kwanza Tanzania imeandika historia kwa kuanza usaili ambao unawafata wasailiwa kule kule kwenye wilaya wanapoishi na kwa kuanza tumeanza na waombaji wa kada ya TEHAMA na baadae waombaji wa kada zote pia watakuwa wakifanya usaili huo kwa njia hiyo ya kidigitali.

Mhe. Simbachawene aliongeza kuwa usaili wa kidigitali unasaidia sana kuwaondolea gharama watoto wa maskini ambao awali walikuwa wanashindwa kuja kufanya usaili kwa sababu tu hawana fedha za kusafiri, malazi na chakula lakini hivi sasa kila msailiwa ataweza kufanya usaili akiwa kwenye eneo jirani na anapoishi na akimaliza atarudi nyumbani.

Usaili huo wa kwanza kufanyika kidigitali hapa nchini umefanyika kila Mkoa na umeanza kwa kada ya TEHAMA ambapo wasailiwa wamefanyia katika maeneo wanayoishi tofauti na awali ambapo walikuwa wakilazimika kutumia gharama kusafiri kwenda mikoa mingine kwa ajili ya usaili huo.


Akizungumzia usaili huo wa kidigitali, Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Bwana Innocent Bomani alisema usaili wa kidigitali unafanyika katika vituo maalum vya usaili vilivyopo kila mkoa ambapo baadhi ya vituo hivyo ni Vyuo Vikuu, Taasisi za Umma zenye maabara za kompyuta na Shule mbalimbali za umma na binafsi.



*Naibu Katibu Miundombinu ya TEHAMA Bi. Mtage Ugulum akifafanua jambo kuhusu Usaili Kidigitali kwa Mhe. Waziri George Simbachawene na Kaimu Katibu wa Sekretarieti ya Ajira Bw. Innocent Bomani*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene akifatilia namna usaili kidigitali unavyofanyika, waliombatana naye ni Kaimu Katibu wa Sekretarieti ya Ajira Bw. Innocent Bomani na Naibu Katibu (Miundombinu) Eng. Mtage Ugulum na Mkuu wa Chuo cha VETA Babati Bi Nansanga Massangya. Wilayani Babati Mkoani Manyara.*



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete akiwa na Mkuu wa Idara ya TEHAMA, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Eng. Samwel Tanguye wakifatilia usaili kidigitali unavyofanyika katika chuo cha Mtakatifu Joseph jijini Dar es Salaam*

# Sekretarieti ya Ajira yashiriki Maonesho ya Biashara Muungano




***Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe.Hemed Suleiman Abdulla.***

Mwaka huu Tanzania imetimiza miaka 60 ya Muungano na maadhimisho yake yameenda sambamba na wiki ya maonesho jijini Dar es salaam ambapo taasisi za Muungano zilishiriki ikiwemo Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

Maonesho hayo yalifunguliwa Aprili 19 mwaka huu ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Hemed Suleiman Abdulla.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa maonesho hayo Makamu wa Pili wa Rais alizipongeza taasisi zote zilizoshiriki maonesho hayo kwa kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi na kuahidi kuwa serikali itaendelea kuuenzi Muungano.

“Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuuenzi na kuulinda Muungano, na Muungano wetu umechangia kuimarika kwa huduma za kijamii kwa pande zote mbili za Muungano, huduma kama vile za maji safi na salama, afya, elimu, ustawi na Maendeleo ya Jamii” alisema.

“Makazi, Usafiri, na kukua na kuimarika kwa uchumi kulikotoa fursa za kibiashara na ajira kwa wananchi. Hivyo ninawapongeza sana na ninawakaribisha wananchi wote kufika katika mabanda haya kujifunza juu ya Muungano wetu” aliongeza.
Aidha, Mhe.Abdulla aliwapongeza washiriki kwa kutoa huduma bora na kuendelea kuelimisha juu ya masuala ya Muungano na kuwataka kuendelea kufanya hivyo ili wananchi wapate uelewa mzuri kuhusu masuala ya Taifa lao.




***Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe.Hemed Suleiman Abdulla akisalimiana na wananchi waliohudhuria maonesho.***

Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kama sehemu ya Taasisi za Kimuungano ilishiriki maonyesho hayo na kuwaeleza wadau juu ya shughuli zote zinazofanywa na taasisi hiyo pamoja na kutoa huduma papo hapo kwa wadau wenye changamoto mbali mbali.

Akizungumza katika maonesho hayo Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bi.Lynn Chawala alisema kuwa ofisi hiyo itaendelea kudumisha Muungano kwa kuhakikisha inatoa huduma bora kwa wananchi wote kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi yetu.

“Ofisi yetu ni moja ya taasisi ya Muungano, na katika kipindi hiki tukiadhimisha miaka 60 tunajivunia kuwa sehemu ya taasisi zinazochagia kuimarika kwa muungano wetu, kwa kuwa wananchi wa pande zote za Muungano wamekuwa wanufaika wa shughuli zetu” alisema.

Aidha, Bi.Chawala aliongeza kuwa ofisi hiyo ambayo jukumu lake kubwa ni kuendesha mchakato wa ajira katika utumishi wa umma imekuwa ikitekeleza jukumu hilo kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu.

“Tunaendesha mchakato wa ajira kwa taasisi za muungano na zile zisizo za muungano, kupitia hilo wananchi kutoka Tanzania bara na Zanzibar wote wamekuwa wakipata fursa hizo kulingana na vigezo vyao” alisisitiza.

Sambamba na hayo, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira ilitumia fursa hiyo kuelezea mfumo mpya wa usaili kidijitali (Online Aptitute Test System – OATS) kwa wateja wake, ambapo wasailiwa hawata safiri umbali mrefu kufuata vituo vya usaili wa mchujo kwani kwa sasa usaili utafanyika katika mikoa na wilaya walizopo ndani ya vituo maalumu
Maadhimisho ya Muungano mwaka huu yalipambwa na kauli mbiu ya “Miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Tumeshikamana na Tumeimarika, kwa Maendeleo ya Taifa” huku maonyesho ya Muungano yakikamilika Aprili 25, 2024.



# Miaka 60 ya Muungano: Waziri Simbachawene aipongeza Sekretarieti ya Ajira

Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene amesema kuwa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imeshiriki kwa kiasi kikubwa kudumisha Muungano katika utekelezaji wa majukumu yake.

Waziri Simbachawene aliyasema hayo jijini Dodoma katika hotuba yake ya kuelezea mafanikio ya Wizara anayoiongoza katika kuadhimisha miaka 60 ya Muungano.




*Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe.George Simbachawene akizungumza na Waandishi wa Habari jijini Dodoma.*

Waziri Simbachawene aliongeza kuwa serikali imeweka utaratibu wa muda wa mgao wa ajira uliokubalika kutumika ambao ni asilimia 79 kwa Tanzania Bara na asilimia 21 kwa Tanzania Zanzibar na kusisitiza kwamba utaratibu huo unatekelezwa kwa mujibu wa Waraka wa Serikali wa tarehe 10 Mei, 2013.

"Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Sekretarieti ya Ajira, imekuwa ikitoa fursa sawa za ajira kwa wananchi wote wa Tanzania ambao wanaomba ajira na kuwa na vigezo stahiki kama elimu, uzoefu na sifa husika" aliongeza.

Aidha, Waziri Simbachawene alibainisha kuwa ili kuwafikia wadau na walengwa wa ajira kwa haraka na kwa gharama nafuu, katika kipindi cha miaka 60 ya Muungano, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, imejenga mfumo wa kidijitali wa ajira serikalini ujulikanao kwa jina la 'Ajira Portal' unaopatikana kupitia tovuti ya www.ajira.go.tz na pia kwa njia ya aplikesheni.

Katika kuendelea kuimarisha ushirikiano, Waziri Simbachawene amesema kuwa katika kipindi cha miaka 60 ya Muungano, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imekuwa ikifanya kazi na Tume ya Utumishi wa Umma Zanzibar inayoratibu masuala ya ajira kwa watumishi wa umma ili kurahisisha zoezi la kutangaza nafasi za kazi na kuwafikia waombaji walio wengi kwa haraka zaidi.

"Katika kuimarisha zaidi Muungano wetu, wataalam wa rasilimaliwatu hasa wanaojihusisha na masuala ya ajira, kwa nyakati mbalimbal wamekuwa wakibadilishana uzoefu na ushirikiano huu umekuwa chachu ya kuendelea kudumisha Muungano wetu kwa kupata watumishi wenye sifa na weledi wa kutosha" alisisitiza.

Katika hatua nyingine Waziri Simbachawene alibainisha kuhusu hatua kubwa iliyofikiwa na Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma ya kuunda mfumo rafiki wa kufanya usaili kidijitali unaotatua changamoto nyingi kwa wananchi wa pande zote za Muungano.

"Kipindi hiki cha miaka 60 ya Muungano, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imedhamiria kuondoa changamoto nyingi zinazowakabili waombaji wa fursa za ajira nchini kwa kuendesha usaili wa kuandika/mchujo Kidijitali kwa lengo la kuwafikia waombaji wote mahali popote walipo Tanzania bara na Zanzibar na ili kukabiliana na changamoto zilizokuwepo, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imesanifu na kujenga mfumo wa kufanya usaili kwa njia ya kielektroniki na mfumo huo umekamilika na umeanza kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa".

Waziri Simbachawene alisisitiza kuwa mfumo huo mpya wa usaili ni wa muhimu kwa kuwa umelenga kurahisisha zaidi mchakato wa ajira hususani kwa wananchi masikini ambao hapo awali walilazimika kusafiri kwa ajili ya usaili lakini kwa wakati huu usaili huo unafanyika karibu kabisa na maeneo yao wanayoishi.



## Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano atembelea Star TV kutoa elimu ya Mchakato wa Ajira



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bi. Lynn Chawala akitoa elimu kwa umma kupitia Star TV*



*Mtangazaji wa Star TV Bernard James akisikiliza kwa umakini majibu na elimu kwa umma kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bi. Lynn Chawala.*

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bi. Lynn Chawala alitembelea kituo cha televisheni cha Star TV cha jijini Mwanza kuzungumza na Watanzania juu ya mchakato wa ajira unavyoendeshwa.

Bi. Lynn Chawala alikuwa mgeni mwalikwa kwenye kipindi cha Tuongee Asubuhi kilichorushwa na kituo hicho tarehe 23 Februari 2023 ambapo mada kuu ya kipindi ilikuwa ni Mchakato wa Ajira Serikalini.

Aidha katika mahojiano Bi. Lynn Chawala aliwataka waombaji kazi kuzingatia masharti yanayotolewa kwenye matangazo ya ajira na kujiandaa vizuri kabla ya kufika kwenye usaili.

Bi Chawala aliwataka wasailiwa kuwa makini dhidi ya wimbi la matapeli ambao wamekuwa wakiwapigia simu wasailiwa na kuwaomba rushwa wasailiwa wakidai wanaweza kuwasaidia kupata kazi na kusema kuwa taarifa zote rasmi za Sekretarieti ya Ajira hutolewa kupitia tovuti rasmi ya www.ajira.go.tz na barua huchukuliwa ofisini Dodoma eneo la Dkt. Asha Rose Migiro (UDOM).



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bi. Lynn Chawala akitoa elimu kwa umma kupitia Star TV akiwa na watangazaji wa Star TV kwenye kipindi wakijadili mchakato wa Ajira*

## Watumishi wa Sekretarieti ya Ajira wapewa mafunzo ya PEPMIS



Kaimu Katibu Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw. Innocent Bomani amewataka watumishi wa ofisi hiyo kuzingatia mafunzo ya mifumo mipya ya Upimaji utendaji kazi kwa Taasisi (PIPMIS) na Mfumo wa upimaji utendaji kwa watumishi wa umma (PEPMIS).

Bw.Bomani ameyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya mifumo hiyo yaliyotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora jijini Dodoma.

Katika ufunguzi huo, Kaimu Katibu amewasihi watumishi wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kujifunza kwa makini na kuelewa vipengele vyote muhimu vya mifumo hiyo.

"Nitoe wito kwenu viongozi pamoja na watumishi

wote msikilize, muulize maswali na muelewe vizuri mafunzo haya kwa sababu msipoelewa kunaweza kuwa na shida huko mbele" alisema.

Aidha, Kaimu Katibu ameongeza kuwa mifumo hiyo (PEPMIS na PEPMIS) ni matokeo ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali inayoongozwa na Dkt.Samia Suluhu Hassan ili kuongeza tija ya utendaji katika Utumishi wa umma.

"Serikali imetumia gharama kubwa kutengeneza mifumo hii kwa hiyo tusifanye mzaha kwenye zoezi hili tujifunze vizuri" aliongeza Bw.Bomani. Katika hatua nyingine Kiongozi huyo amewakumbusha watumishi wa Sekretarieti ya Ajira kuhusu maelekezo yaliyotolewa na serikali kwa watumishi ambao hawatatumia mifumo hiyo.

"Mifumo hii ni muhimu sana kwa sababu inapima matokeo ya utendaji kazi kwa mtumishi wa umma na utendaji kazi wa taasisi na maelekezo yameshatolewa na mamlaka kwa ambao wamefanya mzaha kwenye mifumo hii kusitishiwa mishahara na nisingependa mtumishi kwenye taasisi yetu asimamishiwe mshahara kwa sababu ya kutotekeleza hili la PEPMIS". Sambamba na hayo Bw.Bomani ameongeza kuwa mifumo hiyo itarahisisha masuala mbalimbali ya kiutumishi hususani kwenye upandaji wa madaraja kwa watumishi wa umma.



***Kaimu Katibu Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw. Innocent akizungumza na watumishi wa wa PSRS, kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu Bw. Beni Kalage***

Mifumo huu (PEPMIS) ni mbadala wa mfumo uliokuwepo awali (OPRAS) ambao kutokana na changamoto zilizokuwepo kwenye mfumo huo ikiwemo baadhi ya Watumishi kujaza taarifa zisizo na uhalisia serikali ikaamua kutengeneza mfumo mpya ili kutafuta changamoto hizo.



***Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma akiwa na maafisa habari Nasri Kitwana na Beatrice Kimwaga wakifatilia mafunzo ya PEPMIS***



***Mkuu wa Idara ya TEHAMA Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Eng. Samwe Tanguye, (wa pili kutoka kushoto) na Naibu Katibu Miundombinu ya TEHAMA, Mselem Chengula wakifatilia mafunzo ya PEPMIS***






***Watumishi mbalimbali wa Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma wakifatilia mafunzo ya PEPMIS***

# Kitengo cha Mawasilino chashiriki mafunzo ya eGa jijini Arusha




*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bi. Lynn Chawala akipewa maelezo baada ya kutembelea banda la Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kwenye kikao kazi cha nne cha mamlaka hiyo katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC).*




Kitengo cha Mawasiliano cha Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kimeshiriki katika Kikao Kazi cha 4 cha Serikali Mtandao kilichofanyika kwa siku tatu kuanzia Februari 06 hadi 08, mwaka 2024 katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC) jijini Arusha.

Mgeni rasmi alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mh. George Simbachawene.

Mhe. Simbachawene alisema Serikali imeahidi kuendelea kusimamia na kuhakikisha matumizi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma yanaimarika zaidi, ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kurahisisha upatikanaji wa huduma za Serikali kwa wananchi kidijitali.

Aliongeza kuwa, Sera ya Taifa ya TEHAMA ya Mwaka 2016, inasisitiza juu ya Serikali kutumia fursa zitokanazo na TEHAMA pamoja na matumizi sahihi na yenye tija ya Mifumo ya TEHAMA, katika kuboresha utendaji kazi wa taasisi, unaosaidia kutatua changamoto za kiutendaji, kudhibiti mapato ya Serikali, kujenga na kuboresha uwezo, pamoja na kuimarisha mawasiliano miongoni mwa wadau wa Serikali.

Alibainisha kuwa, Wizara yake imepewa dhamana ya kuratibu na kusimamia matumizi ya TEHAMA Serikalini ili kuhakikisha dhamira ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. ya kuijenga Serikali Mtandao inatimia, kwa kuhakikisha huduma zote za Serikali zinapatikana kidijitali na kuwawezesha wananchi kupata huduma hizo kwa urahisi, haraka na kwa gharama nafuu mahali walipo.

# Kamati ya Ukaguzi yamtaka mkandarasi wa jengo la PSRS kukamilisha ujenzi kwa wakati



*Kamati ya Ukaguzi na baadhi ya viongozi wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma wakiwa katika picha ya pamoja mbele ya jengo la taasisi linaloendelea kujengwa jijini Dodoma*

Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Bw. Mathias Abisai ameiongoza kamati hiyo kufanya ukaguzi wa ujenzi wa jengo la taasisi hiyo unaoendelea katika eneo la Tambukareli NCC Link Jijini Dodoma pamoja na kufanya kikao na Mkandarasi anayejenga jengo hilo ambaye ni kampuni ya CRJE (East Africa) na kuitaka kuongeza kasi ili kuweza kukamilisha ujenzi huo kwa wakati.

Ujenzi wa jengo hilo utakapokamilika utaiwezesha taasisi hiyo kuongeza ubora wa utoaji huduma kwa umma ikiwemo kuendesha usaili na mchakato wa ajira kwa ujumla kwa kuweza kuwahudumia watu wengi zaidi kwa wakati mmoja.

Mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Rais,Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ulianza Aprili, 2022 kwa kumtafuta na kumpata mshauri elekezi wa Mradi ambaye ni Chuo Kikuu cha Ardhi, kupitia kampuni yake ya ushauri elekezi ijulikanayo kama Aru Built Environment Consulting Company LTD (ABECC) aliyepatikana kwa njia ya ushindani. Mshauri mwelekezi alipewa kazi ya usanifu wa Jengo





na kusimamia ujenzi wake hadi kukamililka.

Baada ya usanifu, zabuni ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi ilitangazwa mwezi Septemba, 2022 kupitia zabuni Na. PSRS/2022/W/26: IE/033/2022 -2023/ HQ/W/04 ambapo jumla ya kampuni tano (5) zilishindanishwa ambazo ni; M/s. LI JUN Development Construction Company Limited, M/s. Group Six Intaernational LTD(GSI), M/s Home Africa Investment Cooperation Limited, M/s. CRJE(EAST AFRICA) Limited na M/s HAINAN International Ltd.

Hatimaye mkandarasi wa Kampuni ya CRJE (EAST AFRICA) LIMITED alishinda zabuni na kupewa kazi hiyo tarehe 11 Januari, 2023

Ujenzi wa jengo hili la ghorofa sita la Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ulianza rasmi tarehe 27 Januari, 2023.

Aidha, jengo hili limezingatia miundombinu ya kuwawezesha watu wenye mahitaji maalum (walemavu na wazee) kufika ndani ya jengo bila usumbufu wowote.

Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma una thamani ya jumla ya shilingi 15,430,336,875.94/=

kukamilika kwa jengo hili kutapunguza gharama kubwa ambazo zitatumika katika kukodisha kumbi kwa ajili ya shughuli za usaili.

Pia, jengo hili litasaidia kutoa huduma muhimu kwa wasailiwa wenye mahitaji mbalimbali kama chakula, matibabu ya huduma ya kwanza na mahali pazuri pa kupumzika wakati wakisubiri kushiriki kwenye usaili.

## Watumishi wa Sekretarieti ya Ajira wapewa mafunzo ya NeST



Watumishi wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma wamepewa mafunzo ya Sheria ya Ununuzi wa Umma pamoja na mfumo mpya wa ununuzi Serikalini "NeST"

Mafunzo hayo yameendeshwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) jijini Dodoma.

Mfumo mpya wa manunuzi wa kielekroniki National e-Procurement System of Tanzania (NeST) ulianzishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ukiwa na lengo la kusaidia kudhibiti rushwa, mchakato wa zabuni kuchelewa na kuongeza uwazi wa zabuni.

Mfumo huo uliobuniwa na kutengenezwa na watanzania wenyewe umeanza kufanya kazi ukichukua nafasi ya mfumo wa awali wa TANePS.

## Matukio katika picha: Watumishi wa Sekretarieti ya Ajira katika mafunzo ya NeST











# Ni Huzuni, Simanzi na vilio kila kona, PSRS ikiondokewa na mtumishi Janeth Saki



*Aliyekuwa mtumishi wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, marehemu Bi. Janeth Saki*




*Kaimu Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Bw. Innocent Bomani akiweka shada la maua kumuaga marehemu Bi Janeth Saki*



*Watumishi wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma katika picha ya pamoja baada ya kumpumzisha mpendwa wao marehemu Bi. Janeth Saki*




Kaimu Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Bw. Innocent Bomani amewaongoza watumishi wa taasisi hiyo, ndugu, jamaa, marafiki na watu mbalimbali kutoa heshima zao za mwisho na kumpumzisha aliyekuwa mtumishi wake Bi. Janeth Saki ambaye alifariki tarehe 4 Februari 2024.

Bi. Janeth alifariki katika Hospitali ya Mlonganzila jijini Dar es Salaam alipokuwa akipatiwa matibabu.

Mazishi yalifanyika tarehe 7 Februari 2024 jijini Dar es Salaam.

Bi Janeth Saki, aliajiriwa katika Utumishi w Umma Tarehe 28 Juni 2001 kama Katibu Mahsusi Daraja la III katika Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia wakati huo ambapo alihudumu katika Ofisi hiyo na Ofisi nyingine kabla ya kuhamishiwa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma mnamo Tarehe 13 Februari 2013.

Bi Janeth alihudumu katika Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma tangu 2013 hadi mauti yalipomfika Februari 04, 2024 akiwa na Cheo cha Mwandishi Mwendesha Ofisi Mkuu Daraja la II.

Bwana alitoa, na Bwana ametwaa; Jina la Bwana na libarikiwe.

## Matangazo mbalimbali












## Viongozi wa Sekretarieti ya Ajira watembelea vyombo vya habari kutoa elimu wa umma



Mkuu wa Idara ya TEHAMA Eng Samwel Tanguye na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Bi. Lynn Chawala wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma katika kutoa elimu kwa umma kuhusu mchakato wa ajira unavyoendeshwa walitembelea kituo cha Radio cha A-fm cha jijini Dodoma, Machi 27, 2024.

Kipindi hicho kiligusia zaidi namna Sekretarieti ya Ajira ilivyofanya mageuzi katika uendeshaji wa usaili wa kuandika au mchujo kutoka kwenye kuandika hadi kuhamia kwenye kufanya usaili kwa njia ya mtandao kupitia mfumo mpya ujulikanao kama Online Aptitude Test system.

Mfumo huu unawaondolea gharama wasailiwa za kusafiri kwenda kufanya usaili mkoa mwingine kwasababu sasa watafanya usaili mikoani wanapoishi

Mfumo huo mpya unatoa fursa kwa wasailiwa kuepuka gharama walizokuwa wakituma kusafiri kutoka kwenye mikoa wanapoishi na kwenda kwenye mikoa ambayo usaili ulikuwa ukifanyika.

Aidha kwa sasa wasailiwa wanaweza kufanya usaili kupitia vituo maalumu vilivyopo katika wilaya mbalimbali ambavyo vina maabara za kompyuta, alisema Eng. Tanguye

vituo hivyo ni pamoja na vyuo vikuu, vyuo vya kati, shule pamoja na vituo vyenye maabara za kompyuta.

Wasailiwa wanapaswa kuhuisha taarifa zao kwenye akaunti zao za Ajira Portal ili waweze kupangiwa vituo vya usaili vilivyopo jirani na mahali walipo kwa sasa

Pia, baada ya kufanya usaili wasailiwa wanapewa fursa ya kujua na kuyapata matokeo saa moja baada tu ya kumaliza kufanya usaili.



*Mkuu wa Idara ya TEHAMA, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Eng. Samwel Tanguye akijibu hoja za wadau kwenye kipindi*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Bi. Lynn Chawala wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma*





**Viongozi wa Sekretarieti ya Ajira watembelea vyombo vya habari kutoa elimu wa umma**












## Viongozi wa Sekretarieti ya Ajira watembelea vyombo vya habari kutoa elimu wa umma











## Viongozi wa Sekretarieti ya Ajira watembelea vyombo vya habari kutoa elimu wa umma













## Viongozi wa Sekretarieti ya Ajira watembelea vyombo vya habari kutoa elimu wa umma













## Viongozi wa Sekretarieti ya Ajira watembelea vyombo vya habari kutoa elimu wa umma











## Viongozi wa Sekretarieti ya Ajira watembelea vyombo vya habari kutoa elimu wa umma













